

Usi!.. Usi!.. Usi! na sio **Msi!... Msi!.. Msi!..**

Amri za Mungu zinasema **Usiue, Usizini, Usiibe** ... na sio **Msiibe, Msiue, Msizini**... Ikifunua kuwa Mungu anaongea na mtu mmoja mmoja... Anasema na Mimi kivyangu, lakini pia anasema na wewe kivyako... Na hatuambii wote kwa pamoja.

Kutoka 20:13 "Usiue.

14 Usizini.

15 Usiibe.

16 Usimshuhudie jirani yako uongo.

17 Usiitamani nyumba ya jirani yako..."

Siku ya Hukumu, hatutahukumiwa kwa pamoja, kila mtu atasimama peke yake, na kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe..

Wagalatia 6:5 “Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe”.

Na tena kila mtu atatoa habari zake mwenyewe na si pamoja na mwenzake..

Warumi 14:12 “Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu”

Sasa kama ni hivyo kwanini Boss wako akukoseshe?..kwanini Rafiki akukoseshe, kwanini wanadamu wakukoseshe??... Na ilihali utasimama peke yako siku ile.

Kumbuka unapofanya uzinzi, siku ile hutakuwa na yule aliyefanya naye uzinzi, badala yake utasimama wewe kama wewe (*kwasababu ile amri inakuhusu wewe, na Mungu alikuwa anazungumza na wewe kivyako na si wewe pamoja na mwenzako*)..

Kama unaiba, siku ile hutasimama na aliyekushawishi ukaibe, au uliyekuwa unashirikiana naye katika wizi.. wewe utakuwa peke yako, na yeye peke yake....kwasababu Amri ya **Usiibe**, uliambiwa wewe, nimeambiwa mimi na si wewe pamoja na mimi... Hivyo kila mtu atatoa habari zake mwenyewe.

Kama unaua, ni hivyo hivyo, kama uwaheshimu wazazi ni hivyo hivyo, na amri zote ni hivyo hivyo..

Hukumu ya Mungu inatisha!.

Bwana atusaidie.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya **WHATSAPP**, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Je! sisi kama watakatifu tunaowezo wa kuamuru hukumu?

**WATAMTAZAMA YEYE AMBAYE WALIMCHOMA; NAO
WATAMWOMBOLEZEA.**

**NI WAKATI GANI SHETANI ANAPENDA KUMSHAMBULIA
MWAMINI?**

Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe;

CHUKUA MZIGO WA MWINGINE.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp